


## BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI



### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAOMBI YA UDAHILI KWA MUHULA WA MACHI, 2019

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi katika vyuo vinavyotoa mafunzo kwa ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada ambavyo si Vyuo Vikuu au Vyuo Vikuu Vishiriki nchini. Mojawapo ya majukumu ya Baraza ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi yanakidhi vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Baraza linapenda kuufahamisha umma kuwa **Udahili** wa wanafunzi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa kozi zote isipokuwa Ualimu utanza kutoka tarehe **15 Januari, 2019 hadi tarehe 20 Februari, 2019**. Udahili katika Muhula huu wa Machi, 2019 utahusisha vyuo vyote vilivyo na nafasi na uwezo wa kupokea wanafunzi wapya. Vyuo vya Serikali vinavyotoa mafunzo katika sekta ya afya havitahusika na udahili huu.

Aidha, wahitimu wote wa Elimu ya Sekondari na Vyuo wenye sifa za kujiunga na kozi za Astashahada na Stashahada wanataarifiwa kutuma maombi yao ya kudahiliwa moja kwa moja vyuoni. Waombaji watako chaguliwa na vyuo watakavyomba watawasilishwa NACTE kwa ajili ya uhakiki kabla ya kufahamishwa kujiunga na mafunzo. Masomo kwa watako chaguliwa na kuhakikiwa yataanza tarehe **5 Machi, 2019**.

Baraza lina shauri vyuo na taasisi zote zitakazo dahili wanafunzi kwa Muhula wa Machi, 2019 kuhakikisha kuwa wanazingatia taratibu za matukio ya udahili kama zilivyo kwenye Kalenda ya Udahili (Admission Calendar) inayopatikana kwenye tovuti ya Baraza.

Pia Baraza linawashauri waombaji na wazazi kuhakikisha kuwa wanaomba kwenye Vyuo vilivyokidhi ubora ambavyo vimeorodheshwa kwenye Kitabu cha Mwongozo wa Udahili kwa mwaka 2018/2019 (Admission Guidebook for 2018/2019).

Mwongozo wa Udahili unapatikana katika tovuti ya NACTE: [www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz).

**IMETOLEWA NA:**  
**OFISI YA KATIBU MTENDAJI**  
**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)**  
**TAREHE: 11/01/2019**